

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA
MKUTANO WA MWAKA WA WAGANGA
WAKUU WA MIKOA NA WILAYA ULIOFANYIKA
KATIKA UKUMBI WA NASHERA-MOROGORO
– TAREHE 08 – 12, 2014**

Imetayarishwa na: Sekretariat ya Kamati ya Maandalizi

Imewasilishwa na: Dkt Charles G Massambu, AgDCS

Dondoo za Mkutano ---1/2

A: Utekelezaji kwenye Mikoa na Halmashauri

- 1) Utangulizi
- 2) Mlipuko wa Ugonjwa wa Ebola
- 3) Upatikanaji wa Dawa Vituoni
- 4) Matumizi ya Mtandao wa TEHAMA kwenye utoaji wa Huduma za Afya
- 5) Matengenezo ya Vifaa Tiba
- 6) Ujazaji wa Takwimu Sahihi za Sekta ya Afya
- 7) Kuimarisha Upatikanaji wa Mapato
- 8) Utoaji wa Fedha za Serikali kwa CDH/VAH
- 9) Usimamizi wa Tiba Mbadala

Dondoo za Mkutano ---2/2

B: Utekelezaji Makao Makuu

- 1) Matengenezo ya Magari kupitia TEMESA
- 2) Kuondoa Mkanaganyiko wa Maagizo toka WAUJ na TAMISEMI
- 3) Mgao wa Fedha za CDG kwa ajili ya Mradi wa MMAM
- 4) Akaunti Namba 6
- 5) Upatikanaji wa Dawa Vituoni
- 6) Matumizi ya Mtandao wa TEHAMA kwenye utoaji wa Huduma za Afya
- 7) Usimamizi wa Tiba Asili na Tiba Mbadala
- 8) Michoro ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya
- 9) Ajali za Bara barani na Vituo kuingia Gharama
- 10) Usamabazaji wa Madaktari Bingwa

A: Utekelezaji kwenye Mikoa na Halmashauri

- Utangulizi
- **Mikoa 17 (68%)** iliwasilisha taarifa kwa wakati: Dodoma, Singida, Kagera, Lindi, Tabora, Arusha, Iringa, Simiyu, Mwanza, Rukwa, Shinyanga, Mara, Katavi, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Manyara.
- **Mikoa 6 (24%)** iliwasilisha taarifa kwa kuchelewa: *Kigoma, Tanga, Mtwara, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Geita*
- **Mikoa 2 (8%)** haijawasilisha taarifa: Pwani na Morogoro

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
1.	Mlipuko wa Ugonjwa wa EBOLA	Kila Mkoa/ Halmashauri itayarisha maeneo ya dharura/ Isolation ward kwa ajili ya ugonjwa wa EBOLA kwa kuzingatia mwongozo wa WHO.	<p>Mikoa 16 ilitayarisha maeneo ya dharura kwa ajili ya ugonjwa wa Ebola. Chini ni maelezo kwa kila mkoa uliotekeleza azimio hili:</p> <p>Kagera: Yaliandaliwa maeneo ya dharura matatu: Kituo cha Nshambya - Manispaa ya Bukoba, Bunazi - Wilaya ya Missenyi Rukole - Wilaya ya Ngara.</p> <p>Lindi: Halmashauri zote (100%) zimetenga maeneo ya muda Halmashauri ya Nachingwea wametenga kasma kwa ajili ya jengo la kudumu</p> <p>Tabora: Halmashauri ya wilaya ya Urambo imeandaa Isolation Ward</p> <p>Singida: Manispaa ya ilitenga wodi maalumu kwa ajili ya Ugonjwa wa EBOLA katika Hospitali ya Mkoa wa singida.</p> <p>Wodi maalum zilitengwa katika Hospitali ya St. Carolus Mtinko hospital, hospitali ya Manyoni na hospitali ya Kiomboi (Iramba).</p> <p>Dodoma: Hospitali zote nane (8)katika Halmashauri za Mkoa wa Dodoma zimetenga “Isolation ward” kwa ajili ya magonjwa ya kuambukiza. Mkoa pia ulitenga eneo jingine na jengo maalum nje kidogo ya mji katika Manispaa ya Dodoma kwa ajili ya ugonjwa wa EBOLA endapo ungetokea</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Arusha: Mkoa umeshatenga eneo la kudumu lenye ukubwa wa hekta 3.5 kwa ajili ya magonjwa ya milipuko eneo la Gomba estate. Eneo la kutibu kwa dharura kwa sasa limetengwa katika Kituo cha Murara kilichoko Halmashauri ya Meru.</p>
			<p>Iringa: Mkoa umetenga wodi ya “Isolation” katika Hospitali ya Rufaa. Mkoa unatafuta eneo la kujenga kituo cha kuwatenga wagonjwa wa milipuko na kujenga kulingana na mwongozo wa WHO. Halmashauri za wilaya ya Iringa, Iringa Manispaa, Kilolo, Mafinga Mji na Mufindi zimetenga maeneo maalum kwenye vituo vya kutolea huduma.</p>
			<p>Simiyu: Halmashauri zote (100%) zimetenga maeneo ya dharura/isolation ward kwa ajili ya ugonjwa wa EBOLA</p>
			<p>Mbeya: Halmashauri zote (100%) zimetenga maeneo ya dharura kwa ajili ya ugonjwa wa Ebola.</p>
			<p>Mwanza: Halmashauri zote (100%) zimeshatenga maeneo (isolation & treatment wards). Hata hivyo maeneo yaliyotengwa hayakidhi Viwango vinavyohitajika kwa ajili ya “Treatment and Isolation center” kulingana na viwango vya Shirika la Afya Duniani.</p> <p>Mkoa umepata eneo katika Wilaya ya Ilemela kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha kudumu (Ebola Treatment and Isolation Center). Changamoto -kutoa fidia kwa wananchi na pia fedha kwa ajili ya ujenzi.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			Rukwa: Mkoa na halmashauri zote za Rukwa zilitenga maeneo hayo ndani ya maeneo ya kutolea huduma na baadhi nje, ila hayakuendelezwa kutokana na tatizo la fedha.
			Shinyanga: Maeneo ya dharura yalitengwa katika Manispaa ya Shinyanga katika jengo lililokuwa linatoa ‘huduma za mama ngojea’ Halmashauri ya Kahama TC kwenye jengo linalotarajiwa kuwa kituo cha Afya.
			Mara: Maeneo NANE (8) ya dharura yalitengwa katika Hospitali za Wilaya/Mkoa kwa ajili ya wagonjwa wa Ebola.
			Katavi: Mkoa wa Katavi umetayarisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya magonjwa ya milipuko, ikiwemo Ebola, katika kila Halmashauri ya Mkoa wa Katavi. Halmashauri zote zimetenga fedha katika bajeti ya mwaka 2015/16 kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo.
			Ruvuma: Halmashauri zimeteteleza azimio hili kwa hatua mbalimbali zikiwemo. Halmashauri za Nyasa na Songea wametenga maeneo kwenye vituo viwili (kituo cha Afya cha Muhukuru- Songea na Mbamba Bay- Nyasa). Halmashauri za Songea Manispaa, Mbinga, Namtumbo na Tunduru zimetumia majengo yaliyopo kwa kubadili matumizi

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Manyara: Halmashauri za Babati TC, Babati DC na Simanjiro (Naisinyai) Mbulu (uwanja wa uhuru), Hanang na kiteto zimetenga eneo maalum kwa ajili ya kupokelea wa wagonjwa wa ebola iwapo halmashauri hizo zitapata wagonjwa.</p>
			<p>Njombe: Mkoa wa Njombe umeripoti kutokutekeleza azimio hili kutokana na ufinyu wa bajeti na kutokupatiwa mwongozo wa WHO.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
2.	Upatikanaji wa Dawa Vituoni	Waziri aliagiza kuwa asilimia 50 ya bajeti ya Dawa katika Halmashauri/ Mikoa ipelekwe Bohara ya Dawa (MSD) ili kuijengea uwezo wa kuagiza dawa na Vifaa Tiba mara	Azimio hili halikutekelezwa na Mikoa yote isipokuwa Mikoa ya Rukwa, Katavi, Ruvuma na Mbeya.
		Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iandike barua TAMISEMI ili kutoa maelekezo kwa Sektretarieti za Mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa kupeleka asilimia 50 ya makusanyo ya pesa (NHIF, CHF, TIKA na papo kwa papo) kwa MSD kwa ajili ya manunuzi ya dawa,vifaa tiba na vitendanishi kulingana na maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu	<p>a) Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikupokea maelekezo yoyote kwa maandishi kuhusuana na agizo hili toka OWM-TAMISEMI</p> <p>b) Makusanyo kutoruhusu kuwa na ziada ya kupeleka asilimia 50 kwa MSD. Kwani makusanyo yanapopatikana yote hutumika kununua mahitaji yanayotakiwa kwa wakati huo.</p> <p>c) MSD kuwa tayari na pesa kwa ajili baadhi ya vituo na kushindwa kuvipatia vituo husika mahitaji yao ya dawa na vifaa</p>
		Taarifa za utekelezaji ziwasilishwe TAMISEMI kila baada ya robo mwaka nakala ipelelekw Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.	Hata hivyo, Halmashauri zote zimeripoti kuendelea kutumia asilimia kubwa ya makusanyo yao kununua dawa na vifaa tiba toka MSD, na kununua nje ya MSD pale tu ambapo MSD wanapokuwa hawana mahitaji yao.

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
3.	Matumizi ya Mtandao wa TEHAMA kwenye utoaji wa Huduma za Afya	<p>i) Kila Halmashauri/ Mkoa wafanye maandalizi ya kutumia mtandao wa TEHAMA katika utoaji wa Huduma kwa kuandaa miundombinu husika (computer, local network system).</p>	<p>Mikoa yote iko katika hatua mbalimbali za kutekeleza azimio hili kama ifuatavyo:</p> <p>Kagera: Hospitali Teule za Wilaya za Karagwe, Muleba, Missenyi na Biharamulo tayari zimefanya maandalizi ya vifaa. Hospitali ya Mkoa inaendelea na maandalizi ya kupata vifaa.</p> <p>Lindi: Hospitali ya Rufaa ya Mkoa imeanza kutumia Mfumo wa computer katika kukusanya mapato na hata madaktari kuingiza taarifa za wagonjwa.</p> <p>Tabora: Idara ya afya katika halmashauri ya wilaya ya Urambo imenunua computer tatu kwa ajili ya Hospitali ya wilaya ya Urambo kama maandalizi ya kutumia mtandao wa TEHAMA katika utoaji wa Huduma.</p>
		<p>ii) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaandaa mfumo mmoja utakaotumika kwa ajili ya nchi nzima.</p> <p>iii) Mikoa na halmashauri zinatakiwa kuwasiliana na WAUJ kabla ya kuanzisha mifumo mipya.</p>	<p>Singida: Utekelezaji wa matumizi ya mfumo wa TEHAMA haujaanza kutekelezwa katika Halmashauri zao Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida vifaa vimekwisha simikwa na mafunzo kwa watumishi watakaotumia mfumo huu yanaendelea.</p> <p>Dodoma: Hospitali ya Rufaa ya Mkoa imekamilisha maandalizi ya kutumia mtandao wa TEHAMA katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato na utoaji wa Huduma kwa kuandaa miundombinu husika computer, local network system.</p> <p>Mkoa pia umeanza kusimika mfumo huo wa TEHAMA kwa kutumia kampuni za GPITG LTD na Business Connexions LTD.</p> <p>Katika ngazi ya Mamlaka za Halmashauri utaratibu haujaanza rasmi wako kwenye maandalizi</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Arusha: Halmashauri ya Jiji imetenga fedha kwenye bajeti ya 2015/16 kwa ajili ya manunuzi ya computers.</p> <p>Halmashauri ya wilaya ya Monduli DC imeshaongea na Benki ya CRDB kwa ajili ya kufunga mtandao wa kukusanyia mapato</p>
			<p>Iringa: Maandalizi ya kutumia mtandao wa TEHAMA katika utoaji huduma yamekamilika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa;</p> <p>Julai, 2015, Mkoa kwa kushirikiana na Hospitali ya TUMBI Kibaha imefunga mtandao wa majaribio katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa kutumia “Local network system”.</p> <p>Halmashauri zote za Mkoa wa Iringa ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.</p>
			<p>Mbeya: Halmashauri ya Wilaya za Mbeya jiji, Chunya, Kyela, Ileja, Mbarali, Busokelo, Mbozi na Rungwe zimeanza maandalizi ya matumizi ya TEHAMA; ziko katika hatua mbali mbali za utekelezaji ikiwezo kufanya mazungumzo na wadau, kununua vifaa, kuandaa vyumba.</p> <p>Halmashauri ya Momba haijaanza utekelezaji kwa sababu vituo vingi havina umeme.</p> <p>Aidha Halmashauri ya Mbeya DC haijaanza utekelezaji kutokana na ufinyu wa bajeti</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Mwanza: Hospitali ya Rufaa Mkoa (SekouToure) imeanzisha mfumo wa Ki-elektroniki wa Ukusanyaji wa mapato (GoT-HOMIS). Matumizi haya ya mfumo wa Ki-elektroniki yameongeza mapato kutoka wastani wa 32-40m hadi 49- 50m kwa mwezi. Halmashauri ya Wilaya Kwimba na Magu zilitenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2014/2015.</p>
			<p>Rukwa: Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sumbawanga maandalizi ya awali yameanza na yataendelea jinsi upatikanaji wa fedha utakavyo ruhusu.</p>
			<p>Shinyanga: Hospitali ya Mkoa tayari inatumia TEHAMA katika kukusanya mapato na kutoa huduma za Maabara. Halmashauri ya Msalala DC imeingia mkataba ulioanza mwezi Agosti na Health Promotion and System Strengthening (HPSS) chini ya ufadhili wa serikali ya Uswisi ambayo itasaidia ukusanyaji wa mapato ya CHF kwa kupitia mtandao wa TEHAMA. Halmashauri ya Ushetu DC imeingia mkataba na kampuni ya IWACHU kufunga mitambo ya TEHAMA kwa 2015/2016.</p>
			<p>Mara: Hospitali tatu na vituo viwili vimetekeleza utumiaji wa mtandao wa TEHAMA katika utoaji wa Huduma za Afya. Halmashauri za Tarime Mji na Butiama zimeweka kwenye bajeti ya mwaka 2015/2016 kununua kompyuta kwa ajili ya kusimika mfumo wa “local network system” katika Hospitali ya Tarime na Butiama.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Katavi: Mkoa una Hospitali moja ya Wilaya - (Hospitali ya Wilaya ya Mpanda) ambayo tayari imeshafungiwa mkongo wa Taifa wa TEHAMA. Katika kukamilisha mpango huo, uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda umechukua hatua ya kuingia mkataba na Benki ya CRDB ambayo itafunga mitambo.</p>
			<p>Njombe: Halmashauri za Mkoa wa Njombe zinajiandaa kuanzisha mfumo wa ukusanyaji na udhibiti mapato kupitia TEHAMA, katika mwaka wa fedha 2015/16</p>
			<p>Ruvuma: Halmashauri zote isipokuwa Nyasa, zipo katika hatua za uandaaji wa miundombinu kwa ajili ya kuanza kutumia mtandao wa TEHAMA. Halmshauri ya Wilaya ya Nyasa ina ukosefu wa umeme, hivyo, wanatarajia kuanza maandalizi hayo baada ya kupata umeme wa uhakika mwaka huu wa fedha (2015/2016).</p>
			<p>Manyara: Halmashauri zote zimetenga fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Hospitali zote ziko kwenye hatua mbalimbali za mchakato wa kufunga mfumo wa TEHAMA.</p>
5.			

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
4.	Matengenezo ya Vifaa Tiba	Halmashauri/Mikoa itenge bajeti kwa ajili ya matengenezo ya Vifaa Tiba na kuweka bajeti ya mafundi wa vifaa Tiba kwenye PE. Watumie karakana za kanda kwa ajili ya matengenezo ya vifaa hivyo.	Halmashauri zote zimetenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya vifaa tiba kwa mwaka 2015/2016 katika CCHPs.
5.	Ujazaji wa Takwimu sahihi za Sekta ya Afya	Tatizo la ujazaji/uingizaji wa takwimu sahihi katika mifumo mbalimbali iliyopo, RMOs, DMOs, RSWO na DSWO wasimamie upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati katika sekta ya afya na Ustawi wa Jamii.	Kagera: Mkoa (R/CHMT) kwa kushirikiana na wadau (Implementing Partners –ICAP,MDH na MCSP/Jhpiego) umeweka utaratibu wa kukutana kila robo mwaka kujadili takwimu zilizoingizwa kwenye mifumo mbalimbali ya afya. Lindi: Mkoa umeanzisha utaratibu wa kupitia takwimu zote za afya kila mwezi kabla ya kuwasilishwa Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii Halmashauri pia zina kutana pamoja na wadau wa afya kila robo mwaka kwa ajiri ya kupitia takwimu. afya na Ustawi wa Jamii

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Tabora: Ukusanyaji na uingizaji wa takwimu mbalimbali katika mifumo mbalimbali ikiwemo DHIS na eMIS umeendelea kufanyika kwa wakati na kwa usahihi zaidi kwa usimamizi wa CHMT</p>
			<p>Singida: Baadhi ya watumishi wamepatiwa mafunzo juu ya ukusanyaji, utunzaji na uingizaji wa taarifa katika mfumo wa DHIS2, kabla ya kuingizwa huakikiwa na timu ya RHMT na CHMT, na hivyo kufanya takwimu za mkoa na wilaya kuwa na mapungufu machache ukilinganisha na hapo awali.</p>
			<p>Dodoma: Timu ya afya ya (Mkoa RHMT) inafuatilia kwa karibu suala la takwimu kwenye Halmashauri kwa kufanya yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> a) Vikao vya waratibu wa MTUHA wa Halmashauri na Mkoa vimefanyika viwili tarehe 12-14/12/2014 na tarehe 6-9/07/2015 b) RHMT na CHMT kwa kushirikiana na wadau zimefanya ziara za usimamizi maalumu mbili kwa ajili ya kuhakiki ubora wa takwimu kwenye ngazi ya Halmashauri na Vituo vya tiba. c) Kila CHMT imetenga siku maalum 3-5 za mwanzo wa kila mwezi kwa ajili ya kupokea na kupitia taarifa kutoka kwenye vituo na kuzifanyia masahihisho inavyotakiwa d) WAUJ imekua ikitoa mafunzo rejea mara kwa mara kwa waratibu wa Program mbalimbali ngazi ya Mkoa na Halmashauri

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			Arusha: Ujazaji wa takwimu kwa sasa umeboreshwa kwa kuwa mfumo unaotumika ni wa DHIS na taarifa zinaingizwa kila mwezi kabla ya tarehe 14.
			Iringa: RHMT na Halmashauri zote zina Waratibu wa MTUHA ambaye anafuatilia uingizaji wa takwimu katika DHIS2 na Katibu wa Afya anasimamia uingizaji wa Takwimu katika HRMIS . Waratibu wa MTUHA ambao wanapitia takwimu za Halmashauri zao kabla ya kuziwasilisha mkoani.
			Simiyu: Ukusanyaji wa takwimu kwa kila Halmashauri unasimamiwa ipasavyo
			Mbeya: Ukusanyaji wa takwimu kwa kila Halmashauri unasimamiwa ipasavyo.
			Mwanza: Upatikanaji wa takwimu sahihi za huduma za afya katika ngazi za vituo vya kutolea huduma, Halmashauri na Mkoa umeimarika kwa kiasi kikubwa. Mnamo mwezi Oktoba 2013 upatikanaji wa taarifa mbali mbali kupitia mfumo wa " DHIS2/HMIS TOOLS " ulionesha kuwa Mkoa wa Mwanza ulikuwa nafasi ya pili toka mwisho kwa kuwa na asilimia 44% . Kwa sasa tuna wastani wa 83.38% (Takwimu za 31 June 2015)
			Rukwa: Kwa kutumia mfumo wa DHIS-2 takwimu zinaendelea kuimarika.
			Shinyanga: Halmashauri zimesimamia upatikanaji, uchambuzi na uwasilishaji wa taarifa katika ngazi zote. Mkoa umetoa mafunzo ya ujazaji wa takwimu na kufanya usimamizi saidizi katika vituo vya kutolea huduma.

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Mara: Ukusanyaji na uwasilishwaji wa Takwimu sahihi umeimarika na kuwasilishwa kwa usahihi na kwa wakati katika mfumo wa DHIS2.</p> <p>Mkoa una watumishi 87 wenye mafunzo ya kuingiza na kuratibu takwimu kwenye DHIS. Katika ngazi ya Mkoa kuna waratibu wanne (RHMIS, RRCHco, RIVO na Malaria FP), Kila Halmashauri kuna Waratibu saba (DHMIS, DRCHco, RACC, RIVO, MALARIA FP, DLT, DNO) na Hospitali za Wilaya watatu (Data Clerck, Katibu wa Hospitali na Mganga Mfawidhi).</p> <p>Hospitali zote za Wilaya kuna kompyuta inayotumika kuingiza takwimu.</p>
			<p>Katavi: Mkoa umekuwa ukijitahidi kuhimiza Halmashauri zake kujaza takwimu katika wakati sahihi na kupunguza makosa kwenye takwimu hizo.</p> <p>Kwa mwaka 2014 (JAN-DEC) Mkoa ulikuwa wa pili Kitaifa katika uingizwaji wa data katika mfumo wa kieletroniki (DHIS-2)</p>
			<p>Njombe: Yapo maendeleo mazuri katika ukusanyaji wa takwimu za afya.</p> <p>Uwepo wa maafisa takwimu (M&E officers) waliokuwepo Mkoani imesaidia katika kuboresha takwimu.</p>
			<p>Ruvuma: Halmashauri zote zimelitekeleza azimio hili kwa CHMTs kusimamia upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati katika sekta ya afya na Ustawi wa Jamii.</p> <p>Mafunzo ya usimamizi na ujazaji wa takwimu yalitolewa kwa baadhi ya halmshauri (mfano Songea - Waganga wa vituo 47 walipatiwa mafunzo juu ya “Data CHMTs wakati wa ziara ya usimamizi shirikishi hupitia taarifa na kufanya masahihisho pale panapoonekana kuwa na tatizo.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Manyara: RHMT kila ifanyapo supportive supervision katika halmashauri agenda ya kudumu ni usahihi na matumizi ya takwimu katika utoaji wa maamuzi.</p> <p>Mkoa umekuwa ukitoa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu na kujadili takwimu zipatikanazo katika mfumo wa DHIS2.</p> <p>Mkoa unafanya data audit and validation katika vituo ambako takwimu zinazalishwa na kuwianishwa na zile zilizopo katika mfumo wa DHIS2.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
6.	Kuimarisha ukusanyaji wa mapato	<p>i) Kila Halmashauri/Mikoa iongeze na kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi kwa lengo la kuboresha na kuendesha huduma za Afya na Ustawi wa Jamii</p> <p>ii) Halmashauri zitenge asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji shughuli za afya na ustawi wa jamii</p>	<p>Mikoa iko katika hatua mbali mbali za utekelezaji wa azimio hili.</p> <p>a) Baadhi ya Mikoa imetembelea Hospitali ya Tumbi kujifunza mfumo wa ukusanyaji wa mapato na Takwimu kwa nia ya kuutumia na kuongeza mapato katik vituo vyao. Mfano: Kagera na Tabora</p> <p>b) Baadhi ya Mikoa imefunga mtandao wa komputa na wameanza kutumia mtandao huo ili kuboresha mapato. Mfano; Iringa</p> <p>c) Baadhi ya Mikoa tayari imefanikiwa kuongeza mapato baada ya kutumia mfumo wa komputa na kuwa na usimamizi wa karibu wa ukusanyaji wa mapato. Mfano; Tabora wameongeza fedha kupitia NHIF toka wastani wa tsh 1,300,000/= (2013) hadi tsh 7,000,000/= (2015) kwa mwezi Dodoma kutoka wastani wa Sh 49,768,923 kwa mwezi (2014) hadi wastani wa Sh 89,429,677 kwa mwezi tangu mwezi Machi hadi Julai 2015.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
7.	Utoaji wa fedha za serikali kwa CDH/VAH	1) Halmashauri zisimamie kwa karibu utekelezaji wa sera ya huduma za afya bure kwa makundi ya msamaha kwa Hospitali za CDH/VAH,	<p>Halmashauri zote zenye Hospitali za CDH/VAH zimetokeleza azimio hili. Yafuatayo ni maelezo ya utekelezaji kwa Mikoa yenye Halmashauri zenye CDH/VAH.</p> <p>Kagera: Makundi maalum yanapewa huduma bila malipo katika Hospitali Teule za Wilaya. Kwa mwaka wa fedha 2014/15 Hospitali zilipelekwa fedha za Basket Fund kama ilivyokuwa imepangwa. Mkoa unafuatilia Halmashauri ya Wilaya Bukoba ikamilishe mgao wa fedha kwa Hospitali Teule ya Izimbya.</p> <p>Lindi: Mkoa una hospitali moja iliyoingia mkataba wa CDH na Hospitali 2 zilizo kwenye “Service Agreement” ya kutibu mama wajawazito na watoto. Mikataba yote inasimamiwa ipasavyo na makundi stahili yanapata huduma.</p>
		2) Aidha fedha zipelekwe kulingana na mikataba, na mikataba ipitiwe upya	<p>Tabora: Sera ya huduma za afya bure kwa wazee wasiojiweza, watoto chini ya miaka 5, magonjwa maalumu na mama wajawazito inazingatiwa. Mtaalamu wa kuratibu shughuli za msamaha ameteuliwa kufuatilia sera hii.</p> <p>Singida: Huduma bila malipo zinaendelea kutolewa kwa makundi maalum katika Hospital ya CDH na fedha zinapelekwa kulingana na miongozo Halmashauri zimesainiana mikataba ya utoaji wa huduma na hospitali husika.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Dodoma: Mkoa wa Dodoma una Hospitali teule 2 za St. Gema kwa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Mvumi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino. RHMT zinasimamia kwa karibu na kuhakikisha ya kua Hospitali hizo zinazingatia Sera ya Afya ya kutoa huduma bila malipo kwa makundi ya msamaha. Fedha zinapelekwa kulingana na mikataba kila zinapopokelewa na Halmashauri husika.</p>
			<p>Arusha: Azimio linatekelezwa kwa Halmashauri ya Jiji na Ngorongoro DC. Utekelezaji wa agizo hili katika halmashauri ya Longido DC umekuwa mgumu kwani wamiliki wa Hospitali wanadai kuwa fedha wanazopata ni kidogo, hazitoshi kuendesha huduma ya bure kwa makundi ya msamaha.</p>
			<p>Iringa: RHMT inasimamia kuona Halmashauri zote zenye Hospitali teule (CDH) na mashirika ya dini (VAH) zinatenga fedha kulingana mwongozo wa CCHP na kuzitoa kulingana na bajeti.</p>
			<p>Simiyu: Huduma kwa makundi maalumu kama yalivyoainishwa kwenye sera ya afya zinatolewa bure. Changamoto - uhaba wa dawa.</p>
			<p>Mwanza: Asilimia iliyokubalika toka fedha za wafadhili (basket fund) inapelekwa kwa Hospitali teule ya Sengerema pamoja na Hospitali zenye makubaliano maalumu ya kutoa huduma za Sumve-Kwimba na Bukumbi-Misungwi. Aidha mikataba inapitiwa upya na Halmashauri zinasimamia kuhakikisha sera ya huduma bure kwa makundi maalumu ya misamaha inatekelezwa.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			Rukwa: Agizo hili limezingatiwa katika halmashauri zote za Mkoa wa Rukwa.
			Shinyanga: Halmashauri ya Mji Kahama imepitia mikataba yote kwa vituo vya Afya na Zahanati kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinavyotolewa vinatumika kwa usahihi.
			Mara: Fedha zinapelekwa kwa wakati katika Hospitali za CDH/VAH kadri zinavyopokelewa. Makundi maalumu ya msamaha yanatambuliwa na kupewa huduma kulingana na miongozo. Tofauti na Halmashauri zingine, Halmashauri ya Bunda Pesa zimeendelea kulipwa bila mikataba kwani CDH/VAH haziko tayari kuingia kwenye Mikataba.
			Ruvuma: Halmashauri zote zimeendelea kusimamia kwa ukaribu utekelezaji wa sera ya huduma bure kwa makundi ya msamaha. Aidha, fedha hutolewa kulingana na mkataba (service agreement).
			Manyara: Halmashauri ya wilaya Babati ina CDH na imeingia mkataba na hospitali hii teule ya wilaya na utoaji wa huduma za RCH na wazee ni bure. Changamoto kubwa juu ya utekelezaji wa makubaliano hayo kwani halmashauri zina mikataba na iko kwenye mchakato wa kuingia service agreement kwa kufuata template ya wizara ya afya. Halmashauri ya wilaya ya Simanjiro imepata CDH mwaka huu 2015 na iko kwenye mchakato wa kuingia service agreement

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
8.	Usimamizi wa Tiba mbadala	<p>a) Wizara kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri iondoe mabango na kudhibiti matangazo yanayotolewa kwenye vyombo vya habari yanayohusu Tiba asili ambayo hayafuati sheria , Kanuni na Miongozo ya Tiba ya Asili na Tiba Mbadala.</p>	<p>Kagera: Mabango yaliondolewa. Mkoa kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Tiba Asili na Tiba Mbadala ulifanya kikao na Waganga wa Tiba Asili kuwaelimisha juu ya sheria Tiba Asili na Tiba Mbadala.</p> <p>Lindi: Linatekelezwa, Mkoa na Halmashauri zote zina waratibu wa tiba asilia wanaoratibu na kushughulikia maswala yote ya tiba asilia</p>
		<p>b) Waratibu wote wa Tiba Asili wafanye ukaguzi katika vituo na maduka ya Tiba asili na Tiba mbadala.</p>	<p>Tabora: Mabango yaliondolewa kwa asilimia 60% na kazi ya kuyaondoa yaliyosalia inaendelea. Wakiukaji wa Sheria Kanuni na Taratibu wanaendelea kuchukuliwa hatua ambapo mpaka sasa hivi watu 3 wamefikishwa katika mahakama, mmoja kutozwa faini, mwingine kutoroka baada ya kudhaminiwa, kesi nyingine moja bado inaendelea.</p> <p>Halmashauri ina mratibu wa huduma za Tiba Asili</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			Singida: Ofisi ya mganga mkuu wa mkoa iliwaandikia barua waganga wakuu wa wilaya kupitia Wakurugenzi wa halmashauri, kuhakikisha kuwa hakuna mabango ya waganga wa jadi katika mitaa. Usimamizi umefanyika na maeneo yenye huduma za tiba za asili yametembelewa na kuhakikisha hakuna mabango na matangazo yanayokiuka kanuni.
			Dodoma: Kama hatua ya kwanza mkoa ulianza kwa kuwatambua waganga wa jadi waliosajiliwa na mahali walipo. Mpaka sasa Mkoa una jumla ya waganga wa tiba asili waliosajiliwa 165.
			Arusha: Baraza la Tiba Asili na Tiba mbadala kwa kushirikiana na Mkoa na Ofisi ya RPC walifanya mkutano na watoa huduma za tiba asili na mbadala tarehe 21 Julai 2015 kuhusiana na utoaji wa tiba asili na kuepuka kutoa matangazo na kuweka mabango mitaani.
			Iringa: Mkoa bado haujafanikiwa kuyaondoa mabango na kudhibi matangazo yanayotolewa kwenye vyombo vya habari. Mkoa na Halmashauri umeteuwa Waratibu wa Tiba Asili na Tiba Mbadala. Halmashauri ya wilaya ya Iringa imefanya ukaguzi wa waganga wote wanaotoa tiba asilia na kuwasisitiza kutobandika matangazo yanayohusu tiba asilia hizo. Halmashauri ya Mufindi imefanya ukaguzi wa waganga wote wanaotoa tiba asilia na kuwasisitiza kutobandika matangazo yanayohusu tiba asilia hizo, Halmashauri imefanya usajili kwa Waganga 168 , waganga ambao hawajasajiliwa 117, hivyo wamewapa elimu na utaratibu wa kujisajili. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa wanafanya “supportive supervision” kila robo mwaka. Zoezi la kudhibiti matangazo mbalimbali ya huduma hiyo limekuwa likifanyika kwa kuwatumia Maafisa watendaji wa Kata 18 za Manispaa ya Iringa na kuwahusisha wananchi wote.

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Simiyu: Katika Mkoa wa simiyu ukaguzi unafanyika kwa waganga wote wa tiba mbadala na matangazo yamedhibitiwa. Aidha mkoa bado unaendelea na taratibu za kuwasajili watoa huduma za tiba mbadala.</p>
			<p>Mwanza: Waratibu wa tiba asilia na tiba mbadala wameendelea kufanya ukaguzi katika vituo na maduka ya Tiba asili na Tiba mbadala na kutoa elimu juu ya utoaji wa huduma hizo.</p> <p>Mkoa umesajili Waganga wa Tiba Asili na Tiba mbadala 820 na kutoa mabango yaliyoonekana kukiuka sheria, kanuni na miongozo 112.</p> <p>Waganga waliokiuka taratibu na kukamatwa na vyombo vya dola na kupelekwa mahakamani ni 21.</p>
			<p>Rukwa: Agizo hili limezingatiwa katika halmashauri zote za Mkoa wa Rukwa.</p>
			<p>Shinyanga: Halmashauri za Msalala DC na Kahama TC zimetetekeleza agizo hili.</p> <p>Kwa Halmashauri ya Msalala DC, jumla ya mabango 13 yanayotangaza waganga wa Tiba asili yameondolewa na jumla ya vituo 3 vya tiba mbadala vilifungwa kwa kutokuwa na vibali na kwa kufanya shughuli za tiba mbadala hatarishi.</p> <p>Jumla ya waganga wa asili 73 walitambuliwa na kujaza fomu za kupatiwa leseni za kufanyia kazi zao na walipatiwa elimu ya kuepuka kufanya ramli chonganishi. Halmashauri ya Kahama TC imeondoa mabango na kudhibiti matangazo yanayotolewa kwenye vyombo vya habari yanayohusu Tiba asili ambayo hayafuati sheria , kanuni na miongozo ya Tiba ya Asili na tiba mbadala.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Mara: Halmashauri zote zimetokeleza zoezi la kuondoa mabango na kudhibiti matangazo yanayotolewa kwenye vyombo vya habari yanayohusu Tiba ya asili na tiba mbadala ambayo haifuati sheria, kanuni na miongozo ya Tiba ya Asili na tiba mbadala.</p> <p>Waratibu wa Tiba asili ngazi za Wilaya wanaendelea na zoezi la kuwatambua na kuwasajili na hadi sasa Mkoa wa Mara una Waganga wa tiba asilia 237</p>
			<p>Katavi: Mabango yanayohusu tiba asilia na yasiyozingatia sheria yameondolewa katika Halmashauri ya Wilaya Mpanda na Halmashauri ya Wilaya Nsimbo.</p> <p>Zoezi la kusajili wataalamu wa tiba asilia linaendelea na mpaka sasa wataalamu wa tiba asilia 25 wamesajiliwa katika Halmashauri ya Wilaya Mpanda, na 24 katika Halmashauri ya Manispaa Mpanda. Halmashauri ya Wilaya ya Mlele imehakikisha wataalamu wote wa tiba za asili wanatambulika, wanasajiliwa na kupewa vibali kulingana na taratibu za tiba za asili zilizowekwa pamoja na kuthibiti mabango yasiyofuata sheria.</p>
			<p>Njombe: Uondoaji wa mabango umekuwa mgumu kwani unahitaji ushirikiano wa hali ya juu kati ya idara, wataalamu wa tiba asili / mbadala na jeshi la polisi.</p> <p>Tunashauri Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itoe matangazo ya mara kwa mara kupitia redio / mass media kuhusiana na suala hili</p>
			<p>Ruvuma: Mabango yanayohusu Tiba asili na tiba mbadala ambayo hayafuati sheria , kanuni na miongozo ya Tiba ya Asili na tiba mbadala yameondolewa. Mfano; Halmashauri ya wilaya Songea imeondoa mabango yapatayo 8 ambayo yalikuwa yamening'inizwa barabarani mbali na sehemu ya kutolea huduma. Aidha, waganga watano (5) waliobainika kutokuwa na vibali vinavyowawezesha kutambua tiba asili ambayo haitafuati sheria. Njira za kuifanya sheria kuifanana na sheria za tiba asili.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
			<p>Manyara: Mkoa una mratibu wa Tiba asili na tiba mbadala, vilevile Halmashuri zote zina waratibu wa Tiba ya Asili na tiba mbadala ambao wamepewa mafunzo na Baraza la tiba asili na tiba mbadala.</p> <p>Mkoa kwa kushirikiana na Baraza la Tiba asili na Tiba mbadala umefanya usimamizi shirikishi katika halmashauri zote za mkoa na kufanya mkutano na waganga wa tiba asili na kuwahamasisha juu ya usajili na kudhibiti utoaji wa huduma kinyume cha sheria ikiwa ni pamoja na kuondoa mabango na kujitangaza kupitia vyombo vya habari vya ndani ya mkoa</p>

B: Utekelezaji Makao Makuu

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
1.	Matengenezo ya Magari kupitia TEMESA	<p>Kutokana na uwezo mdogo wa TEMESA na kupeleka magari kwa wazabuni waliokuwa wakitumiwa na Halmashauri mwanzoni, inasababisha gharama za matengenezo kuwa kubwa.</p> <p>Hivyo wajumbe waliazimia kuwa ni vizuri utaratibu uliokuwa unatumika awali wa utengenezaji wa Magari utumike badala ya huu wa sasa.</p> <p>Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iwasiliane na Wizara ya Ujenzi ili ifanye tathmini upya kuhusu uwezo wa TEMESA kutengeneza magari ya Serikali.</p>	<p>Ni kweli kuwa TEMESA inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa jukumu lake la utengenezaji wa magari ya serikali kwa ujumla.</p> <p>Wizara ya Ujenzi kupitia wakala wake wa kutengeneza magari ya Serikali, hawana pingamizi kutumia karakana Teule ambazo zimeteuliwa na kushinda zabuni ya kutoa huduma hiyo, na zile ambazo zilikuwa zikitumiwa na Health Sector Reform wakati wa mfumo wa TMIS- Transport Management Information System iwapo ziliteuliwa zinaweza kuendelea kutumika kwa mfumo ule wa awali wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii lakini kwa kufuata miongozo iliyotolewa na TEMESA .</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
2.	Kuondoa mkanganyiko wa maagizo toka WAUJ na TAMISEMI	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wakutane na TAMISEMI ili waweze kukubaliana kuhusu kutoa maagizo yanayoleta mkanganyiko, mfano uratibu wa TIKA/CHF katika ngazi ya Halmashauri, muundo wa Idara ya Usafi na Mazingira na Suala la Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuwa pamoja katika ngazi ya Halmashauri.	<p>Suala la muundo wa Idara ya Usafi na mazingira lilishatolewa ufumbuzi. Maelekezo na mwongozo ulishatolewa na OWM TAMISEMI, hali kadhalika kwa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii.</p> <p>Community Health Fund Protocol imepitiwa na kufanyiwa maboresho na wadau wote walishirikishwa ambapo imeshasainiwa na kusambazwa nchi nzima.</p> <p>Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ipo tayari kufanya review itakapohitajika.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
3.	Mgao wa fedha za CDG kwa ajili ya mradi wa MMAM	TAMISEMI itoe maelekezo kwa Halmashauri ili fedha za CDG zitumike katika kutekeleza MMAM.	<p>Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbambali za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma zikiwamo huduma za Elimu, Afya, Maji na Biashara.</p> <p>Vipaumbele hivyo ni "descretionary" ya wanufaika wa Fedha hizo. Ambao wanapanga shughuli za kutekeleza kwa kulingana na maeneo ya Vipaumbele vyao (Bottom up Aproach) kwa kuzingatia utekelezaji wa dhana ya D by D kwa kupitia uibuaji wa viupaumbele kwa mfumo wa Opportunity and Obstacles to Development (O & OD). Fedha hizo zimekuwa zikitumika katika shughuli za MMAM kwa kipindi chote toka zimenza kutolewa mpaka mwaka huu wa fedha. Aidha kwa takwimu zilizopo Sekta ya Afya ni ya Pili katika sehemu kubwa ya matumizi ya fedha hizo baada ya Sekta ya Elimu.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
4.	Suala la Akaunti namba sita	<p>TAMISEMI iangalie upya suala la kufutwakwa akaunti namba sita ambako kumesababisha kuchelewesha na kutotekeleza baadhi ya shughuli za Idara ya afya.</p> <p>Hii ni kutokana na ukweli kwamba fedha hii ipo kwenye kapu moja la akaunti ya maendeleo ambako wakati mwingine fedha hizo hutumika kwa shughuli zingine zisizo za Idara ya Afya hivyo kuchelewesha utekelezaji wa shughuli za afya na wakati mwingine kutokutekelezwa kabisa utoaji wa taarifa.</p>	<p>Azimio limezingatiwa,</p> <p>OWM - TAMISEMI imekwisha toa Mwongozo kwa Barua ya Terehe 09/07/2015 yenye Kumb. Na. CCE.3/215/01/79.</p> <p>Mwongozo huo umeelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kufungua akaunti mpya tatu zikiwamo Sekta ya Maji, Elimu na Afya na hivyo kufanya kila Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na Jumla ya Akaunti za Benki Tisa (9). Mwongozo huo pia umeelekeza namna ya ufunguaji wa akaunti hizo pamoja na uendeshaji wa Akaunti hizo.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
5.	Upatikanaji wa Dawa Vituoni	<p>Waziri aliagiza asilimia 50 ya bajeti ya Dawa katika Halmashauri/ Mikoa ipelekwe Bohari ya Dawa (MSD) ili kuijengea uwezo wa kuagiza dawa na Vifaa Tiba mara Halmashauri/ Mkoa zitakapoagiza</p> <p>Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iandike barua TAMISEMI ili kutoa maelekezo kwa sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kupeleka asilimia 50 ya makusanyo ya pesa (NHIF, CHF, TIKA na papo kwa papo) kwa MSD kwa ajili ya manunuzi ya dawa,vifaa tiba na vitendanishi kulingana na maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu.</p> <p>Taarifa za utekelezaji ziwasilishwe TAMISEMI kila baada ya robo mwaka nakala ipelelekw Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.</p>	<p>Wizara ilimwandikia DG-NHIF kuanza kukata fedha za malipo ya Bima kutoka hospitali zilizoko fungu namba 52 na kuzipeleka MSD kwa ajili ya kununulia dawa kwa hospitali hizo.</p> <p>Aidha, Wizara imemwandikia KM-TAMISEMI kuviagiza vituo vya kutolea huduma za afya zilivyo chini ya TAMISEMI kutuma kiasi cha asilimia 50 ya mapato Bohari ya dawa ili fedha hizo zitumike kununulia dawa na kuijengea MSD uwezo wa kununua dawa.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
6.	Matumizi ya Mtandao wa TEHAMA kwenye utoaji wa Huduma za Afya	<p>Kila Halmashauri/ Mikoa wafanye maandalizi ya kutumia mtandao wa TEHAMA katika utoaji wa Huduma kwa kuandaa miundombinu husika (computer, local network system), ili kuboresha utoaji wa huduma za afya, ukusanyaji na udhibiti wa mapato katika Vituo vya kutolea Huduma vya Umma</p> <p>Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaandaa mfumo mmoja utakaotumika kwa ajili ya nchi nzima.</p> <p>Hivyo, mikoa na halmashauri zinatakiwa kuwasiliana na WAUJ kabla ya kuanzisha mifumo mipya.</p>	<p>Wizara imeshafanya uchambuzi yakinifu kuhusu mfumo wa kielekroniki unaotakiwa ikiwa ni pamoja na miundombinu inayotakiwa kwa ajili ya maandalizi ya kutumia mifumo ya kielekroniki kwenye hospitali zote za mikoa za rufaa.</p> <p>Aidha, Wizara imeziunganisha hospitali zote za mikoa za rufaa kwenye mkongo wa Taifa (National Fiber Optic) ili ziweze kupata mtandao wa uhakika na kuweza kuwasiliana.</p> <p>Vile vile, Wizara kupitia Shirika la Bima ya Afya (NHIF) ipo kwenye hatua za mwisho za ununuzi wa mfumo huu.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
7.	Usimamizi wa Tiba mbadala	<p>Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri iondoe mabango na kudhibiti matangazo yanayotolewa kwenye vyombo vya habari yanayohusu Tiba asili ambayo hayafuati Sheria , Kanuni na Miongozo ya Tiba ya Asili na tiba mbadala.</p> <p>Aidha waratibu wote wa Tiba asili wafanye ukaguzi katika vituo na maduka ya Tiba asili na Tiba mbadala.</p>	<p>Katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala na Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam, iliondoa mabango 1,128; Halmashauri ya Temeke mabango 248, Halmashauri ya Ilala mabango 580 na Halmashauri ya Kinondoni mabango 300.</p> <p>Aidha, Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa kuzingatia maagizo ya Wizara ilifanikiwa kuyaondoa mabango yote yanayotangaza huduma za tiba asili kinyume na sheria.</p> <p>Baraza limefanya uhamasishaji unaohusu usajili wa waganga wa tiba asili katika mikoa ya Njombe, Singida, Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga na Simiyu.</p> <p>Katika mwaka 2015/16 Julai na Agosti Baraza limefanya uhamasishaji unaohusu usajili wa waganga wa tiba asili katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.</p> <p>Wakuu wa mikoa yote Tanzania bara wameandikiwa barua kuhusu kusimamia usajili wa waganga wa tiba asili katika mikoa yao ikiwa pamoja na udhibiti wa waganga wa jadi wanaojihusisha na mauaji ya watu wenye ualbino.</p> <p>Wizara imeagiza kuwa matangazo yazingatie Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala Namba 23 ya mwaka 2002 katika kutangaza matangazo yanayohusu huduma za tiba asili na tiba mbadala.</p>

Na	Dondoo	Azimio	Utekelezaji
8.	Michoro ya Vituo vya kutolea huduma za afya	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iandae upya michoro ya vituo vya kutolea huduma za afya na isambazwe katika Mikoa na Halmashauri zote.	<p>Kazi ya kupitia mwongozo uliokuwepo imekamilika na kwa sasa maelezo ya mwongozo yameridhiwa na uongozi wa Wizara tayari kwa kuchapishwa.</p> <p>Inashauriwa baada ya hapo, wataalam wa kila eneo la huduma (service area eg. Laboratory, Theatres, Pharmacy) wakae na kutoa mapendekezo mahsusi pamoja na waandaji wa michoro.</p> <p>Wataalam wa Maabara na Famasi tayari wamefanya hivyo.</p>
9.	Ajali za barabani na vituo kuingia gharama	Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii ifanye mazungumzo na Wizara zinazohusika kuhusu umuhimu wa Bima ya vyombo vya usafiri kuchangia gharama za matibabu kwa wanaopata ajali na vifo.	Maoni haya yamezingatiwa katika mkakati wa ugharamiaji wa huduma za afya unaotarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2015

Nawashukuru kwa usikivu wenu

